# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

S.L.P 73
TUNDUMA

24/04/2018

## TANGAZO LA ZABUNI

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA INAKARIBISHA MAOMBI YA ZABUNI KWA WAFANYABIASHARA/VIKUNDI/KAMPUNI NA TAASISI MBALIMBALI ZENYE SIFA NA UWEZO WA UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO KUTOKA VYANZO MBALIMBALI KUTOKA HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**ORODHA YA ZABUNI:**

| UTOAJI WA HUDUMA YA ZABUNI ZA UWAKALA: | | |
|---|---|---|
| 1. | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 01 | Wakala wa kukusanya ushuru wa stendi eneo la Mwaka.(Bus Stand) |
| 2 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 02 | Wakala wa kukusanya ushuru wa madini ya ujenzi mchanga ,mawe, kokoto , kifusi na tofali. |
| 3 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 03 | Wakala wa kukusanya ushuru wa vitunguu , mbogamboga ,mawese na viazi |
| 4 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 04 | Wakala wa kukusanya ushuru wa mpunga ,mchele, pumba laini za mpunga ,pumba laini za mahindi na mashudu. |
| 5 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 05 | Wakala wa kukusanya ushuru wa mazao ya misitu. |
| 6. | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 06 | Wakala wa kukusanya ushuru wa vyoo kwenye masoko yafuatayo:- (i) Soko la mazao (ii) Soko la Makambini (iii) Soko la Majengo ( iv) soko la Mpemba. |
| 7 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 07 | Wakala wa kukusanya ushuru wa maegesho ya magari katika Mji wa Tunduma . |
| 8 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 08 | Wakala wa kukusanya ushuru wa soko la Majengo na Makambini. |
| 9 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 09 | Wakala wa kukusanya ushuru wa magulio na minada katika Mji wa Tunduma. |
| 10 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 10 | Wakala wa kutoza faini za maegesho ya magari katika maeneo yasiyo rasmi (wrong parking) na upitishaji magari mazito barabara zisizoruhusiwa katika mji wa Tunduma. |
| 11 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 11 | Wakala wa kukusanya ushuru wa mahindi, maharage ,ulezi, karanga ,ufuta, mtama, uwele na alizeti. |
| 12 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 12 | Wakala wa kukusanya ushuru wa samaki na dagaa |
| 13 | LGA/167/TTC/2018/19/LOT 13 | Wakala wa kukusanya ushuru wa usafi wa mazingira wa bajaji,pikipiki na pikipiki za miguu mitatu. |

**MASHARTI YA MWOMBAJI YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:-**

1. Halmashauri itasimamia ukusanyaji wa mapato kwa njia za Kielektroniki na mapato yataingizwa moja kwa moja kwenye Akaunti za Halmashauri na malipo ya ada ya ukusanyaji kwa mawakala yatafanywa kwa kutumia asilimia isiyopungua ile iliyoainishwa na Hamashauri kwenye barua ya tuzo.
2. Mwombaji awe ni kampuni/taasisi au vikundi vilivyosajiliwa kisheria Tanzania na sio watu binafsi.
3. Kampuni/Taasisi au vikundi lazima viwe na Leseni ya Biashara, TIN,Hati ya usajili, Ofisi inayotambulika na Tax clearance certificate.
4. Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi kwa mujibu wa mkataba utakaoingiwa na kufuata masharti ya Mkataba
5. Zabuni ambazo zitakuwa hazijapokelewa na kusomwa hadharani siku ya ufunguzi wa Zabuni hazitafikiriwa na bodi ya zabuni.
6. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha, athibitishe kwa taarifa ya Benki (Bank Statement) ya miezi mitatu (3) iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni.
7. Kila mwombaji lazima awe na uwakilishi wa kisheria"Registered Power of Attorney".
8. Ada ya maombi ya Zabuni ni Tsh. **100,000/=** (mia moja elfu tu) ambapo kiasi hicho kitalipwa na kukatiwa Stakabadhi ya malipo ambayo itaambatishwa katika barua ya maombi na fedha hizo hazitarudishwa.
9. Mwombaji aweke picha mbili za rangi "Passport size" za hivi karibuni.
10. Mwombaji awe na uwezo na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema zabuni anayoomba na pia aoneshe vielelezo vya uzoefu wake.
11. Mwombaji anatakiwa kutoa stakabadhi za kielektroniki kukusanyia mapato ambapo vifaa hivyo atapewa na Halmashauri.

**MASHARTI YA NYONGEZA KWA MWOMBAJI WA UWAKALA.**

12. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka kiasi cha fedha taslimu mwezi mmoja kama dhamana yake ya zabuni anayoomba kwa kiasi ambacho kitakubalika na kuelekezwa kwenye barua ya tuzo.
13. Mwombaji awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa na Halmashauri katika sheria ndogo za ukusanyaji wa ushuru.
14. Mwombaji aliyewahi kufanya kazi na Halmashauri na kushindwa kutekeleza masharti ya mkataba kwa njia yoyote hatafikiriwa kupewa zabuni.
15. Mapato yatakusanywa kwa kutumia Mashine za kielektroniki ambazo ni mali ya Halmashauri na ikibainika wakala yuko kinyume na matakwa haya hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
16. Kwa maelezo zaidi ya kupata ufafanuzi fika ofisi za Halmashauri kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kuanzia saa 1:30 Asubuhi mpaka saa 9:30 Alasiri (Jumatatu hadi Ijumaa).
17. Mwombaji ni lazima awe na mashine ya kielektroniki (EFD) atakayoitumia kutoa risiti za fedha za marejesho atakazolipwa na Halmashauri.
18. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kulipia vifurushi vya mashine za kukusanyia mapato.
19. Maombi yote yawasilishwe kwa mkono na kutumbukizwa kwenye sanduku la zabuni lililopo ofisi ya ugavi.
20. Bahasha zenye zabuni zifungwe na lakiri zionyeshe jina na namba ya Zabuni inayoombwa zikielekezwa kwa anuani hii.

KATIBU BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA
S.L.P 73,
**TUNDUMA**

21. Mwisho wa kupokea maombi itakuwa tarehe 16/05/2018 saa 4.00 asubuhi siku ya jumatano na ndio itakuwa siku ya ufunguzi wa zabuni. Waombaji, wawakilishi na watu wote wenye maslahi mnaalikwa kushuhudia ufunguzi wa zabuni tajwa hapo juu. Ufunguzi utafanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma uliopo eneo la Chapwa.

**KASTORI.G. MSIGALA**
**KAIMU MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA.**